TANGAZO LA SERIKALI Na. 429 la tarehe 30/6/2023

SHERIA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# KANUNI

*(Zimetayarishwa chini ya Kifungu cha 29(1)(m))*

KANUNI ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA ZA VISIMA VYA KIBIASHARA NA KIJAMII ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Jina Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA KUSAJILI NA KUFUTA USAJILI

4. Matakwa ya kusajili.
5. Kuepuka migongano kimaslahi.
6. Kufutwa kwa Usajili.

SEHEMU YA TATU
WAJIBU WA WAHUSIKA

7. Wajibu wa Mtoa Huduma.
8. Wajibu wa Mwenye Leseni.

SEHEMU YA NNE
BEI ZA MAJI

9. Utaratibu wa Kuomba Bei.
10. Rufaa.

11. Fidia kwa Miundombinu iliyopo.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

12. Ukaguzi.
13. Makosa.
14. Masharti ya mpito.
15. Adhabu ya Jumla.
16. Mamlaka ya Udhibiti kuwa na uwezo wa kuongeza Taratibu.

MAJEDWALI

SHERIA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

# KANUNI

(*Zimetayarishwa chini ya Kifungu cha 29(1)(m))*

KANUNI ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA ZA VISIMA VYA KIBIASHARA NA KIJAMII ZA MWAKA 2023

## SEHEMU KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Maji na Usafi wa Mazingira, Visima vya Kibiashara na Kijamii1za mwaka 2023.

Matumizi

2.-(1) Kanuni hizi zitatumika kudhibiti uendeshaji wa visima vya kibiashara na kijamii vilivyopo katika eneo la mwenye leseni.

(2) Kanuni hizi hazitamhusu mtu ambaye ana kisima kwa matumizi yake binafsi.

Tafsiri
Sura ya 272

3. Katika kanuni hizi, isipokuwa pale muktadha utakapohitaji vinginevyo:

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira;

Sura ya 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya EWURA;

"kisima" maana yake ni shimo refu au kisima kilicho chongwa chini ya ardhi ili kupata maji.

"Bei elekezi" maana yake ni kiwango cha juu cha bei kwa kila mita moja ya ujazo ya maji, kinachotozwa kwa mteja na mwendeshaji kama kilivyoidhinishwa na EWURA.

"Cheti cha usajili" maana yake ni cheti kinachotolewa na mwenye leseni kwa mwendeshaji wa kisima baada ya kusajiliwa chini ya kanuni 4(6)(a;

"kisima cha kibiashara" maana yake ni kisima kinachomilikiwa au kuendeshwa kwa lengo la kibiashara;

"kisima cha kijamii" maana yake ni kisima kinachomilikiwa au kuendeshwa na kikundi cha watu, mtu binafsi, shirika au taasisi kama za kidini na za hisani au mtu yeyote ambaye anataka kutoa huduma hiyo pasipokuwa na lengo la kufanya biashara;

"mteja" maana yake ni mtu anayepatiwa huduma ya maji kutoka kwa mwendeshaji wa kisima

Sura ya 414 "Sheria ya EWURA" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji;

"kibali cha maji" maana yake ni kibali chochote cha kutengeneza, kuchimba, kupanua, au kuongeza kina cha kisima kinachotolewa na Bodi ya Bonde la Maji chini ya Sheria ya Menejimenti ya Rasilimali za Maji; Sura ya 331

"mkaguzi" maana yake ni Afisa kutoka kwenye Ofisi ya mtoaji leseni au mtu yeyote yule aliyepewa mamlaka hayo.

"mwenye leseni" maana yake ni Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira iliyopewa leseni na Mamlaka ya Udhibiti kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira;

"eneo la leseni" maana yake ni eneo ambayo mtoa huduma ameruhusiwa kutoa huduma za maji na usafi wa Mazingira;

"Wizara" maana yake ni Wizara yenye jukumu la kusimamia shughuli za Maji na Usafi wa Mazingira;

"mtoa huduma" maana yake ni mtu yeyote anayeendesha kisima cha kijamii au kisima cha kibiashara;

"sehemu ya kuhifadhi" maana yake ni miundombinu iliyojengwa au kutengenezwa kutokana na malighafi ambazo haziharibu ubora wa maji yaliyohifadhiwa humo kabla ya kusambazwa;

"Bei" maana yake ni tozo, bei au kiwango kinachotozwa kutokana na huduma ya maji na usafi wa Mazingira kama itakavyoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti;

Sura ya 285 "Baraza" maana yake ni Baraza la Ushindani lililoanzishwa chini ya Sheria ya Ushindani;

Sura ya 331 "kibali cha matumizi ya maji" ina maana ya kibali cha kutumia au kuchepusha, kuengeneza bwawa, kuhifadhi, kuondosha au kutumia maji yaliyo juu ya ardhi au chini ya ardhi kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Menejimenti ya Rasilimali za Maji.

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU WA KUSAJILI NA KUFUTA USAJILI

Matakwa ya kusajili

4.-(1) Hakuna mtu atakayeuza au kusambaza maji katika eneo lililopewa leseni kwa kutumia kisima cha maji isipokuwa kisima hicho kiwe kimesajiliwa na mwenye leseni chini ya kanuni hizi;

(2) Bila kuathiri matakwa yaliyopo kwenye kanuni ndogo ya (1), mtoa huduma aliyekuwepo kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, katika kipindi cha miezi 12 baada ya Kanuni hizi kuanza kutumika, atatuma maombi ya kusajili kila kisima kwa mujibu wa masharti Kanuni hizi.

(3) Maombi ya usajili yatakayofanywa chini ya kanuni ndogo za (1) na (2) yatakuwa katika mfumo ulioainishwa kwenye Jedwali la Kwanza na yatajumuisha taarifa zifuatazo:

(a) jina kamili la mwombaji, anuani ya biashara, namba za simu, barua pepe na tovuti (kama ipo);
(b) maelezo ya kifundi ya kisima chenyewe;
(c) kibali halisi cha matumizi ya maji;
(d) nakala halisi za vipimo zinazothibitisha ubora wa maji vilivyofanywa na Mamlaka zinazohusika au Maabara zinazotambulika; na
(e) malipo ya gharama za usajili kama zilivyoanishwa na mwenye leseni ambazo hazitazidi shilingi za kitanzania laki mbili.

(4) Mwenye leseni, baada ya kupokea maombi chini ya kanuni ndogo ya (3) na kujiridhisha na usahihi wa ujazwaji wa fomu za maombi atakagua maombi hayo kwa kuzingatia yafuatayo:

(a) iwapo yanakidhi matakwa ya Sheria;
(b) rekodi za utendaji za mwombaji; na
(c) iwapo maelezo ya kifundi ya kisima yanakidhi matakwa ya kitaalam kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(5) Mwenye leseni baada ya kukamilisha uchambuzi wa maombi chini ya kanuni ndogo (4) ataidhinisha, atarejesha maombi kwa marejeo zaidi au kukataa maombi hayo.

(6) Mwenye leseni-
(a) iwapo amekubali maombi, atatoa cheti cha usajili kulingana na maelezo yaliyotolewa katika Jedwali la Pili; na
(b) pale ambapo amerejesha maombi kwa marejeo au kukataa maombi, atamjulisha mwombaji kwa maandishi ikiwa ni pamoja na kumpa sababu za kurejesha au kukataa maombi.

(6) Pale ambapo mwombaji hataridhika na maamuzi ya mwenye leseni, chini ya kanuni ndogo (6) anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka ya Udhibiti kwa uamuzi zaidi.

(7) Mtoa huduma, baada ya maombi yake kukubaliwa na kupewa cheti cha usajili na Mamlaka husika chini ya kanuni ndogo (6) atatambulika kama Wakala wa mwenye leseni.

(8) Mtoa huduma wakati wote atawajibika kufuata maagizo yote yaliyoainishwa kwenye cheti cha usajili.

(9) Kipindi cha usajili kilichotamkwa kwenye kanuni ndogo (6) kitakuwa miaka mitatu na kinaweza kuongezwa kwa kipindi kingine cha miaka mitatu endapo mtoa huduma ataomba.

(10) Mtu yeyote atakayekiuka matakwa ya kanuni ndogo za (1) na (2) za kanuni ya 4 atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua mwezi mmoja au adhabu zote mbili.

Kuepuka migongano kimaslahi

5.-(1) Hakuna mwajiriwa wa mwenye leseni ambaye ataruhusiwa kutoa huduma za kuendesha visima.

(2) Sheria yeyote inayosemekana kumpa mamlaka

mwajiriwa wa mwenye leseni za usajili itakuwa batili na haitakuwa na nguvu.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka matakwa ya kanuni ndogo (1) atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili.

(4) Kwa madhumuni ya kanuni hii neno "mwajiriwa" lina maana ya mtu yeyote anayefanya kazi katika ofisi za mwenye leseni au mjumbe wa bodi ya wakurugenzi anayetumikia kipindi chake kwa wakati huo.

kufutwa kwa usajili

6.-(1) Mwenye leseni anaweza kufuta usajili wa kisima iwapo atagundua kuwa-

(a) ubora wa maji umepungua na hauendani na viwango vya ubora vinavyotakiwa vya maji ya kunywa nchini Tanzania;
(b) kuendelea kutumia kisima hicho ni hatarishi kwa mazingira, maisha ya watu na mali;
(c) mwombaji ametoa taarifa za uongo au zisizo sahihi kuhusiana na uendeshaji na takwimu za kitaalam kuhusu kisima;
(d) mtoa huduma anauza maji kwa bei za juu zaidi kuliko zile zilizoidhinishwa au mtoa huduma ameshindwa kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

(2) Mtoa huduma yeyote ambaye kisima chake kimefutiwa usajili chini ya kanuni hii ataacha mara moja kutoa huduma na anatakiwa kurudisha cheti cha usajili kwa mwenye leseni na kuacha kutoa huduma ya maji kwa kutumia kisima hicho.

(3) Katika kipindi cha siku saba baada ya kufuta usajili wa kisima, mwenye leseni atamfahamisha mtoa huduma kwa maandishi.

(4) Kisima chochote ambacho kimefutiwa usajili hakitakuwa na sifa ya kusajiliwa tena ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kufutiwa usajili.

(5) Mtoa huduma yeyote ambaye ataendelea kutoa huduma ya maji kutumia kisima kilichofutiwa usajili na mwenye leseni chini ya kanuni ya 6 atakuwa anatenda

kosa na akitiwa hatiani atawajibika kumlipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kutumikia kifungo kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili.

(6) Mtoa huduma yeyote ambaye hataridhika na maamuzi ya mwenye leseni anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka ya Udhibiti kwa uamuzi katika kipindi cha siku tisini baada ya kuarifiwa.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA WAHUSIKA

Wajibu wa mtoa huduma

7. Wakati wote wa uhai wa cheti cha usajili mtoa huduma atafanya yafuatayo:

(a) kusambaza kwa mteja maji safi na salama ambayo yanakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa;
(b) kuhakikisha kuwa mabomba, vifaa na mashine zilizofungwa kwenye kisima ni salama na zinafanya kazi ili kuzuia uchafuzi wa maji wakati wa kuyasambaza kwa wateja.
(c) kutoa ushirikiano kwa mkaguzi ili kufanikisha kazi ya ukaguzi wa kisima;
(d) kuonesha nakala halisi ya cheti cha usajili na kuweka bango karibu na kisima linaloonesha bei kikomo ya maji;
(e) kuweka takwimu za maji yaliyozalishwa kiasi cha maji yaliyouzwa, gharama za uwekezaji na uendeshaji;
(f) kuweka ushahidi wa bei kwa wateja;
(g) kufanya na kutoa taarifa ya vipimo vya ubora wa maji hasa kuhusu *"Ph turbidity, faecal coliforms, fluoride, chuma, manganese na salinity"* kwa mwenye leseni kama itakavyoelekezwa na mwenye leseni;
(h) kwa wakati wote kuhakikisha kuwa kisima kimekidhi matakwa ya kifundi kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Tatu;
(i) kuhakikisha kuwa kisima kina mfumo wa kupima kiwango cha maji;

(j) kukidhi matakwa ya sheria husika ikiwa ni pamoja na vigezo na viwango stahik; nai

(k) kuomba idhini kutoka kwa mwenye leseni kuhakikisha kuwa mahitaji yote ya kitaalam kuhusu upanuzi wa usambazaji maji, ukarabati na kuunganisha wateja, unafanywa kulingana na vigezo vya kitaalam vya mwenye leseni.

Wajibu wa mwenye leseni

8.-(1) Mwenye leseni atahakikisha kuwa wakati wote wa uhai wa cheti cha usajili, mtoa huduma anatekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

(2) Bila ya kujali ujumla wa masharti ya kanuni ndogo (1): mwenye leseni ana jukumu la kufanya yafuatayo wakati wa uhai wa cheti cha usajili;

(a) kukagua ubora wa maji yanayosambazwa na mtoa huduma kwa kuhakikisha kuwa mtoa huduma amefanya vipimo na kutoa taarifa kuhusu ubora wa maji katika maeneo ya *"Ph turbidity, faecal coliforms, fluoride,* chuma*, manganese na salinity*" kama itakavyoagizwa na mwenye leseni;

(b) kuwasilisha kwa Mamlaka ya udhibiti taarifa za utendaji kazi wa watoa huduma kila baada ya robo mwaka;

(c) kushughulikia malalamiko ya wateja kuhusu huduma ya maji inayotolewa na watoa huduma;

(d) kuchunguza mwenendo wa bei ya maji yanayosambazwa na mtoa huduma;

(e) kwa kila mwaka kutoa taarifa kwenye Magazeti ya Kiswahili na kingereza yanayosambazwa sana, orodha ya watoa huduma pamoja na namba zao za simu, anuani zao za biashara na mahali walipo;

(f) kumsaidia mtoa huduma kuzingatia na kufuata matakwa yote ya kitaalam kuhusu upanuaji wa huduma za maji, ukarabati na uungaji wa wateja katika mtandao wa maji kwa kufuata vigezo vilivyowekwa na mwenye leseni; na

(g) kukagua miundombinu na maendeleo ya mtoa huduma angalau mara mbili kwa mwaka.

## SEHEMU YA NNE
## BEI ZA MAJI

Utaratibu wa kuomba Bei

9.-(1) Mwenye leseni anaweza yeye mwenyewe au baada ya kupokea maombi kutoka kwa mtoa huduma, kuwasilisha maombi ya bei za maji kwa Mamlaka ya Udhibiti kama inavyoelekezwa kwenye Kanuni za EWURA za Kukokotoa Maombi ya Bei za Maji.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), mwenye leseni, angalau mara moja baada ya iaka mitatu anaweza kuwasilisha maombi ya kuomba bei ya maji ya visima kwa Mamlaka ya Udhibiti, isipokuwa hakuna ombi la mabadiliko ya bei ya maji litakalofanywa katika kipindi cha miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuidhinisha maombi ya mwisho.

(3) Bila kujali matakwa ya kanuni ndogo ya (2), mwenye leseni anaweza kuwasilisha maombi ya bei ya maji kwa Mamlaka ya Udhibiti wakati wowote ikigundulika kuwa kuna mabadiliko makubwa katika mazingira ya uendeshaji.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mwenye leseni anawajibika kufanya Mkutano wa mashauriano na watoa huduma kabla ya kupeleka maombi ya mapendekezo ya bei kwa Mamlaka ya Udhibiti.

(5) Pasipo kujali ujumla wa kanuni ndogo ya (1), maombi ya bei yataambatana na yafuatayo:

(a) barua kutoka kwa Waziri anayehusika na masuala ya maji kuthibitisha ombi la bei ya maji chini ya kanuni ndogo ya (1);
(b) uthibitisho kwa maandishi juu ya bei zinazoombwa na tarehe ya kuanza kutumika;
(c) kumbukumbu na sahihi za waliohudhuria mikutano ya mashauriano;
(d) maelezo ya kina na mahesabu ya jinsi ya bei hizo zilivyofikiwa yakiwa katika mfumo wa Microsoft na Excel; na
(e) maelezo ya faida ambazo wateja watapata kutokana na bei zinazopendekezwa.

(6) Mamlaka ya Udhibiti baada ya kupokea

maombi chini ya kanuni ndogo (1), itatathimini na kubainisha usahihi wa maombi ya bei na baada ya hapo itafanya uchunguzi wake kwa mujibu wa matakwa ya kifungu cha 19 cha Sheria ya EWURA

(7) Baada ya kukamilisha uchunguzi wake Mamlaka ya Udhibiti itaweka bei kikomo ya maji na kuitangaza bei hiyo kwenye Gazeti la Serikali.

(8) Mamlaka ya Udhibiti, kila robo mwaka itatangaza bei kikomo za maji katika magazeti ya Kiswahili na kiingereza yenye ushawishi mkubwa.

(9) Mtoa huduma yeyote atakayeuza maji juu ya bei kikomo, anatenda kosa akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua mwezi mmoja au adhabu zote mbili.

Rufaa

Sura ya 285

10. Mtu yeyote atakaye kuwa na malalamiko kuhusiana na uamuzi wa Mamlaka ya Udhibiti, chini ya kanuni ya 9(7) anaweza kukata rufaa kwenye Baraza chini ya Sheria ya Ushindani.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Fidia kwa miundombinu iliyopo

11.-(1) Inapotokea kuwa mwenye leseni ana uwezo wa kitaalam na kifedha na akaanza kutoa huduma za maji katika maeneo ambayo yana huduma kidogo au hayana kabisa, watoa huduma wote katika eneo hilo, wataacha kutoa huduma za visima kwa wateja katika eneo hilo, na mwenye leseni kulingana na matakwa ya kanuni ndogo (2), atakuwa na uhuru wa kutumia miundombinu iliyopo ambayo inamilikiwa na watoa huduma hao.

(2) Mwenye leseni, endapo ataamua kutumia kisima na miundombinu inayomilikiwa na mtoa huduma, atawajibika kutoa fidia kwa mtoa huduma huyo katika kiwango ambacho watakubaliana.

Ukaguzi

12.-(1) Mkaguzi anaweza kukagua kisima na taarifa zozote muhimu kwa utoaji wa huduma ya maji, na mtoa huduma atawajibika kutoa msaada unaotakiwa

kuwezesha ukaguzi huo.

(2) Wakati wa ukaguzi, Mkaguzi anaweza kufanya yafuatayo;

(a) Kutoa nakala za mambo muhimu yanayomuwezesha mtoa huduma kutoa huduma za maji; na
(b) Kukagua kisima na miundombinu yote ya kisima ikiwa ni pamoja na mabomba, mashine, mitambo mbalimbali, dira za maji na vikorombwezo vingine muhimu vinavyo tumika katika utoaji maji ya kisima.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo (1) Mamlaka ya Udhibiti, wakati wowote ule inaweza kufanya ukaguzi wa kisima, na kuomba kupewa taarifa zozote muhimu zinazosaidia utoaji wa huduma za maji na kuchukua hatua stahiki kulingana na matakwa ya Kanuni hizi na sheria husika nyingine.

(4) Kama mwenye leseni akibaini kuwa mtoa huduma amekiuka baadhi ya matakwa ya kanuni hizi au sheria husika yeyote, Mwenye Leseni anaweza kutekeleza yafuatayo;

(a) Kuchukua hatua stahiki kama zinavyobainishwa katika kanuni hizi ikiwa ni pamoja na kufuta usajili wa kisima, au
(b) Kuchukua hatua nyingine kama itakavyo onekana inafaa ili kulinda maslahi ya wateja.

Makosa

13. Mtoa huduma ambaye;

(a) atazuia Mamlaka ya Udhibiti au mkaguzi kufanya kazi zake kama inavyobainishwa katika Kanuni hizi na sheria husika;
(b) atakayetishia au kutumia lugha ya matusi kwa mkaguzi;
(c) atakayekataa au kushindwa kutii maagizo halali na maelekezo ya Mkaguzi,
(d) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili.

Masharti ya mpito

14. Mtu yeyote anayetoa huduma ya maji kutumia kisima ndani ya eneo la mwenye leseni katika kipindi cha miezi sita baada ya Kanuni hizi kuanza kutumika, anatakiwa kufanya maboresho katika huduma zake na ukarabati wa kisima na miundombinu yake ili kukidhi matakwa ya Kanuni hizi.

Adhabu ya jumla

15.-(1) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi pale ambapo hakuna adhabu mahsusi ambayo imetamkwa bayana atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini au kutumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu au adhabu zote mbili.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia chini ya kanuni ndogo (1) na akaendelea kutenda kosa lilelile atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na elfu hamsini kwa siku kwa wakati ambao kosa limendelea kutendwa.

(3) Mtoa huduma yeyote anayeajiri wakala, karani, mtumishi au watu wengine atawajibika kwa kila tendo au kosa litakalofanywa na mtu huyo kuhusiana na uendeshaji wa kisima.

Mamlaka ya Udhibiti kuwa na uwezo wa kuongeza Taratibu

16. Pale ambapo hakuna utaratibu uliyobainishwa katika Kanuni hizi, Mamlaka ya Udhibiti itafanya lile linalowezekana chini ya Sheria, Sheria ya EWURA, na sheria nyingine husika kushughulikia suala lolote lililowasilishwa mbele yake

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetayarishwa chini ya Kanuni ya 4(3)*)

**PICHA**

FOMU YA MAOMBI YA USAJILI WA VISIMA VYA MAJI VYA KIBIASHARA NA KIJAMII

Malengo ya maombi ni (weka alama "X" katika kisanduku husika)

(a) Kuomba usajili ☐

(b) Kuomba kuendeleza usajili ☐

(c) Kutoa taarifa ya kubadili umiliki wa kisima ☐

(d) Kutoa taarifa ya kusitisha huduma ☐

(e) Kutoa taarifa ya kubadili maelezo ya usajili ☐

SEHEMU YA KWANZA
MAELEZO YA JUMLA

A. Maelezo ya Mwombaji

1. Jina kamili la Mwombaji (Waombaji)
…………..………………………………………………………………
2. Wadhifa:
…………………………………...………………………………………………………
………….

3. Anuani ya Mwombaji (Waombaji)

Anuani ya Mwombaji
S.L.P……………….

Nyumba Na. ……………. Kiwanja Na. ………………… Kitalu Na. …………… Mtaa ……………………………..….

Jiji / Manispaa / Mji ………………………………………………..

Simu Na. …………………………………… Simu ya Mkononi Na. …………………

Barua pepe ………………………………………… Tovuti …………………………

B. Hadhi ya kisheria ya Mwombaji (weka alama "X" sehemu husika)

Binafsi ☐ Kampuni ☐ Ubia ☐

Asasi isiyo ya Serikali ☐ Jumuiya ☐

C. Taarifa za Kiufundi
Namba ya kibali cha kuchukua maji …………………………………… Uwezo ($m^3$)………………………….

Mahali kisima kilipo ……………………………………………………………………………

Mkoa ………………..…… Jiji/Manispaa/Mji ………………..… Kata………………… Mtaa/Kijiji ………………….

SEHEMU YA PILI
SEHEMU HII IJAZWE KWA AJILI YA TAARIFA YA KUBADILI UMILIKI WA KISIMA TU

Mimi ………………………………………………………. wa S.L.P …………………… ninatoa taarifa kwamba nimebadili umiliki wa kisima kwenda kwa ………………………………………………………………. wa S.L.P …………. kuanzia …………………………….. siku ya …………………….

SEHEMU YA TATU
SEHEMU HII IJAZWE KWA AJILI YA TAARIFA YA KUSUDIO LA KUSITISHA HUDUMA

Mimi ……………………………………………………………………………... wa S.L.P …………………………. Ninatoa taarifa kwamba nimesitisha kusambaza huduma ya maji kwa kisima katika eneo la ……………………………………………………., kuanzia …………….. siku ya …………… 20…………….

SEHEMU YA NNE
SEHEMU HII IJAZWE KWA AJILI YA TAARIFA YA KUBADILI MAELEZO YA USAJILI

Mimi ……………………………………………………………………….. wa S.L.P ……………………………….. Ninatoa taarifa kwamba nimebadili maelezo yangu ya usajili kama ifuatavyo kutoka (jaza maelezo ya sasa ya usajili) ………………………………………………………………… kuwa (jaza maelezo mapya ya usajili)………
Kuanzia …………………………. Siku ya …………………… 20……………….

SEHEMU YA TANO
NYARAKA ZINAZOWASILISHWA PAMOJA NA FOMU YA MAOMBI

Mambo ya kuangalia (weka alama ya vema sehemu husika)

1. Nakala zilizothibitishwa za vipimo vya ubora wa maji ya kisima ☐

2. Taarifa ya kiufundi ya kisima ikijumuisha vipimo na vifaa vilivyotumika katika ujenzi

3. Ushahidi wa malipo ya ada ya maombi ☐

4. Taarifa za ukaguzi, matengenezo na ukarabati ☐

5. Kibali cha kuchukua maji ☐

SEHEMU SITA
KIAPO CHA MWOMBAJI (WAOMBAJI)

Mimi / sisi (*futa lisilohusika*), nili/tuliosaini hapa chini, nina/tunakiri kwamba, maombi haya yote, matamko yote yaliyofanyika, viambatanisho vyote na taarifa zote zilizowasilishwa kwa ajili ya maombi haya, kwa utashi wangu/wetu ni kweli, sahihi na kamili kwa vigezo vyote na matakwa yote.

Mimi / sisi (*futa lisilohusika*), nina/tuna elewa kwamba (Weka jina la Mamlaka) wanaweza kufanya uchunguzi kamili wakina kupata usahihi wa maelezo yote yaliyotolewa humu ndani na Mimi/ sisi (*futa lisilohusika*), tunaipa (Weka jina la Mamlaka) mamlaka ya kufanya uchunguzi huo.

Mimi / sisi (*futa lisilohusika*), nina/tunawapa mamlaka wafanyakazi wangu / wetu kutoa maelezo yoyote kama ambavyo kwa sababu zozote yanahitajika na (Weka jina la Mamlaka) kuhusiana na maombi haya.

| Mwombaji | Shahidi (Kamishna wa Viapo) |
|---|---|
| Jina kamili ………………………… | Jina kamili ………………………… |
| Wadhifa: …………………………… | Wadhifa: …………………………….. |
| Saini: ……………………………………. | Saini: ………………………………… |
| Tarehe: …………………………………….. | Tarehe: ……………………………….. |

SEHEMU YA SABA
KWA MATUMIZI YA OFISI TU

1. Je muombaji (waombaji) ame (wa) mesajiliwa na (Weka jina la Mamlaka) kama mtoa huduma ya maji?

   Ndio ☐ Hapana ☐

2. Je fomu za maombi zimejazwa kwa ukamilifu na kusainiwa na Ofisa aliyethibitishwa na muombaji?

   Ndio ☐ Hapana ☐

3. Je muombaji amekidhi matakwa ya usajili wa kutoa huduma ya maji kwa jamii?

   Ndio ☐ Hapana ☐

   Tarehe ya Kupokea: ……………………………….. Imepokelewa na: ………………………

Nambari ya Mwombaji: ………………………………… Saini: ……………………………
Muhuri wa Ofisi

___________

JEDWALI LA PILI

___________

(*Imetayarishwa chini ya Kanuni ya 4(b)(a)*

(Weka logo ya Mwenye leseni)
Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira

CHETI CHA USAJILI WA KISIMA CHA KIBIASHARA NA CHA KIJAMII

CHETI NAMBARI ……………….

Cheti cha usajili wa Kisima cha Kibiashara/kijamii kimetolewa kwa ……………………… wa sanduku la posta ………………… kutumia/kuendesha kisima namba ………………. Barabara ……………………… Wilaya …. Kwa ajili ya kutoa huduma za maji kuzingatia vigezo na matakwa yaliyopo kwenye kiambatisho.

Cheti hiki kitaanza kutumika kuanzia …. Siku ya …………..,20 … na kitaendelea kutumika kwa kipindi cha miezi kumi na mbili (12), labda kifutwe au kuongezewa muda kama inavyoelekezwa katika Kanuni za maji na Usafi wa Mazingira (Kanuni za Huduma ya Maji Kutoka Visima Binafsi vya Maji), 2021

Tarehe ya kutolewa ……………….

…………………….
Mkurugenzi Mtendaji

_____________

JEDWALI LA TATU

_____________

*(Limetayarishwa chini ya Kanuni ya 7(h))*

Mahitaji ya Kiufundi ya Kisima cha Maji

Kisima cha maji kinatakiwa kiwe:

(a) Kiwe mahali ambapo ni rahisi kufikika kwa aili ya kufanya ukaguzi, matengenezo, maboresho ya mitambo, kusafisha maji na kupima ubora wa maji.
(b) Kisiwe ndani ya mzunguko wa mita 50 kutoka majosho ya ng'ombe, vyoo, mashimo ya maji machafu na sehemu nyingine hatari. Uchafu kutoka kwenye mashimo utupwe upande wa chini wa kisima ili kuzuia uchafuzi wa maji.
(c) Kiwe na kina cha mita kumi na tano
(d) Kichinbwe kwenye maeneo ambayo hakuna mafuriko wakati wa mvua au uchafuzi wa maji yanayotiririka na kijengwe kuepuka kuchafuliwa na mafuriko
(e) Kijengwe sehemu yenye mwinuko kuepuka uchafuzi wa maji.

*Tangazo la Serikali Na. 429 (Linaendelea.)*

(f) Kiwe kimezungushiwa zege yenye upana wa centimita 15 na upana wa kisima uwe angalau sentimita sitini (60) pande zote za kisima kutoka katikati ya mfuniko.

(g) Mfuniko wa kisima uwe angalau sentimita thelasini juu ya zege na chini la kisima

(h) Kama pampu ya kutumbukiza majini itatumika, mfuniko wa kisima lazima uzibwe kikamilifu ili usiruhusu maji kuingia na ustahilimi mitikisiko au misukosuko ya 'conductors or cables'

(i) Kuwe na mfumo wa mabomba ya kutolea maji:

- (i) Ulio na mabomba ya kufunga na kufungua (*check valve, shutoff valve, pressure gauge*) na mita ya maji ya kupima mwenendo au mtiririko wa maji; na
- (ii) Wenye 'raw meter sampling tap' kabla ya bomba la kutolea maji kutoka kwenye kisima; na
- (iii) Iwe imeunganishwa na sehemu ya kuhifadhia maji.

Dodoma, ........................., 2023

JAMES A. MWAINYEKULE,
*Mkurugenzi Mkuu*